# SHAWISHI LINAOZINGATIA ARDHI YENYE UHAI

## *Kukuza Amani Katika Maisha Yote*

*"Katika mazung'umzo yetu yote si budi tutilie maanani matokeo ya mawazo yetu kwa vizazi saba zijazo."*
— Hekima ya Iroquois

## UANZILISHI

Matatizo ya dharura yanayohusu walimwengu yanaweza kutatuliwa na mpangilio uliyoyaleta. Watu wa tamaduni na umri mbali mbali wanajitokeza kote ulimwenguni kuitisha mabadiliko maalum kuhusu tunavyojipanga kama watu.

Mamilioni na makundi wanashughulikia suluhu ya kudumu na yenye utu. Katika andamano ya ulimwengu kubwa na iliyo na utafauti, kuna ukubaliano kwamba tuko na fikara; ujuzi; mawazo; uvumizi na rasilimali. Vivyo hivyo; uongozi wenye maarifa kusuluhisha janga mbali mbali zinazokidhiri. Tatizo letu la kimsingi ni kuyalainisha na kuyapanga mambo vilivyo kwa ajili ya uponyaji wa nchi na mabadiliko au mageuzo ya mradi mzima.

Kuhakikisha mchanganyiko uliotosha duniani kote, kuhusu hekina na suluhisho, ni muhimu kwamba sisi binaadamu, tukomboe uthibiti na mamlaka yetu binafsi na hata ya pamoja ili tujipange katika mambo yanayotuhusu (utawala, sharia, uchumi, elimu na kadhalika) kwenye hali ya maisha na hali ya ubinaadamu inayojibuka kila mara.

Kulingana na ada hii, sisi walimwengu tunaungana katika wazo la kuponya ulimwengu anayosaidia kikamilifu mipangilio ya watu kwenye mitaa na ulimwengu kote kwa minajili ya kufikia mahitaji na fikara yetu kuhusu ardhi yenye uhai.

## MSIMAMO

Sisi, walimwengu, tunaungana kwa upendo na kusumbukia dunia tunamoishi pamoja na vyumbe vyote. Tunaungana kama jamii moja kupita mipaka ya inchi mbali mbali, tamaduni na mawazo; kurejesha ubora wa maisha kwa dunia yote.

Tunatambua kwamba, uhai wetu binafsi na wa pamoja kama walimwengu umeungana na unategemeana. Ili binaadamu kukua ni lazima mazingara ya dunia yote izingatiwe kuendelezwa.

Tunahimiza ya kwamba wajibu rasimi wa uongozi ni kulinda na kukuza afya na uendelezi wa ulimwengu an vyumbe vyote vilivyomo kwa vizazi vijavyo.

KWA HIVYO, sisi, wanainchi wa ulimwengu, tunaapa kujipanga kwa hatua ya haraka na ya kudumu. Tunajitolea kufanya kazi pamoja na vikundi vidogo na vya asili ; na huduma za kibinafsi ; pamoja na vikundi vya imani mbali mbali, serikali za mitaa, taifa na kimataifa pamoja na biashara na mashirika ya kifedha kufanya yafuatayo:

1. Kugeuza hali yote ya maisha vilivyo ili ilete uponyaji na hashima pamoja na mwelekeo mwema wa maisha yote.
2. Kurejesha uasili na afya pamoja na utafauti wa vyumbe vyote.
3. Hakikisha binadamu wote na wanyama waweza kufikiana na mahitaji yao ya dharura kutokana na hakikisho la uwepo wa:
   - i. maji safi
   - ii. hewa safi
   - iii. mchanga wenye uhai
   - iv. vyakula mbali mbali
   - v. pahali pema pa kuishi
   - vi. usalama wa kimwili na kiakili
   - vii. hali na mali ya kitamaduni nay a kiulimwengu yanayoitajika ili kutambua uwezo wa kibinafsi katika hali ya kujijazia utajiri katika vijiji na ulimwenguni.
4. Kuza uelewano wa hali zote uliokubaliwa kuhusu matatizo yetu ya pamoja, suluhu zilizopo na njia kamilifu za uponyaji.
5. Ungano la kuunda endelezo lililoshirikianwa kiulimwengu ili kuwa na tamaduni lenye amani, huruma, utiifu, umoja katika utafauti wetu, hekima, uajibikaji, ushirikiano, urejesho wa uzazi na unyenyekevu wa maisha yote.

## NJIA MWONGOZO

Tunajitolea kwa njia ya mwongozo ufuataο kama msingi unaohitajika katika mageuzi ya mtumo wote kupona ambao unahitajika kwa haraka nyakati hizi:

### Kutokuwepo vita na Usimimizi

- Twajitahidi kutosababisha kuumia na kupanga mawazo yetu, maneno na matendo na yale mambo yanayojenga jamii yote.

- Zingira, heshimu na rejesha mambo ya kimsingi maishani kama vile dunia, maji, hewa, moto, hali ya anga, mabadiliko kwenye anga na hali ya maisha kawaida.
- Zingira na heshimu binadamu asili na nchi yao kisha unganisha mitumo ya ushauri wao, maarifa na hekima katika vipengele vyote vya hali za binadamu.
- Hakikisha makubaliano yote yanazingatia msimamo wa matokeo kwa afya ya kila kitu kwenye vizazi saba vijavyo, na kwamba kundi zote za vitu vilivyo vya jamii ya binadamu na visivyo vinawakilishwa na kuzingatiwa.

## Umoja katika Tofauti

- Heshimu na sikiza sauti za watu walioachwa nyuma katika kutengeneza pamoja mwongozo wa jinzi ya kuenda mbele.
- Hakikisha kuzingirwa kikamilifu na usawa wa watoto wasichana pamoja na wanawake katika maisha ya watu wote.
- Endeleza kuelewa kwetu kuhusu mambo muhimu na hali za lazima za binadamu na vyiumbe mbalimbali.
- Kuza tamaduni za kuwa na watu wote ambao hufuraia tofauti zetu mbalimbali zinazoboresha maisha.
- Kubaliana na vipengele vya ndani vya binadamu, tamaduni na mambo yanayotatiza mazingira na kazi kuanzisha uponyaji kamili na njia waafaka za kurejesha hali ya kawaida zinazozingatia hasa jamii zilizoathiliwa zaidi, vizao na anga zote.

## Uchumi na Sheria

- Kutoa kubaliano kwa sharia zinazotunza na kuleta maisha upya na kukana sharia zote zinazo ruhusu maisha kuumia.
- Ekeza mali kwa yale mambo yanayotunza na kuleta maisha upya na kurudisha mali yaliyoekezwa katika mradi wowote unaodhuru au unayoweza kudhuru maisha.
- Hakikisha viwanda na miradi inayodhuru maisha inaungwa mkono ili ibadilishwe au iondolewe kabisa.
- Sababisha hali mwafaka za mahitaji muhimu ya binadamu na wanyama kufikiwa tunapotazama kuelekea kwenye uchumi na miradi iliyo na afya.

## Elimu, Masomo na Mawasiliano

- Eleza wanainchi kila mahali kuhusu tatizo za kiulimwengu na za vijiji, yale yanayosabisha tatizo hizo, na utajiri wa suluhu zilizo kuwepo, jaribio mbalimbali na mitandao kutoka kwa sehemu zote zilizotunukiwa ubinafsi, upamoja na uponyaji na ugeuzi wa ulimwengu na mageuzi.
- Tambua, endeleza na inua uponyaji na nafasi za kujifunza ukuaji kwa watu wa umri wote, kujifunza njia mbalimbali, yanayopendelewa na uwezo, ili kuunga mkono unawilisaji wa mtu binafsi, watu wote na vitu vyote kwa jumla.
- Ekeza hekima, na sayanzi za mitumo ya kufikiria na mitumo kamilifu ya afya na uponyaji..

- Anzisha upya lugha yetu, uwezo wa matamshi, kujieleza kiujuzi na hadithi za kitamaduni ili kukuza watu waliokua na ujuzi, ufahamu, huruma, watendaji na wanaopenda kusaidia.

## Kubadili Kuelekea Mitumo Mipya Ya Maisha

- Hakikisha ya kuwa watu walio na vyeo vya uongozi wana ujuzi katika kutumia mwelekeo wa mtumo kamilifu wa afya na uponyaji, pamoja na kuzingatia kikamilifu maadhiri ya uaminifu, ustadi, huruma, hekima, kujitolea, utendaji, ujuzi na kujiachilia kwa ajili ya manufaa ya kila kyumbe.
- Anzisha endelezo la mtandao unaowezesha kujifunza, kuweka pamoja, kuunda vyema na kueneza sharia za ubinifu maalum zilizoko, sera na mazoezi ya mtumo kamili wa afya na uponyaji kwenye sehemu zote, na kuunda njia mbalimbali ili kuchukuliwa ili kutumika kotekote ulimwenguni kulingana na mahitaji na hali ya jamii asili.
- Panga teknolojia na maendeleo ya kisayansi ili kuwezesha afya na uponyaji wa mtumo kamili.
- Kuza mpangilio wa kibinafsi uliongozwa na hekima pamoja na ujuzi wa vyongozi wa wanainchi kutoa mawaidha kuhusu sera zenye hekima na zinazoweza kupeana suluhu mwafaka katika hali ya kuzingatia mahitaji,rasilimali na utegemeanaji wa waasika walio binadamu na wasio binadamu.
- Unda na anzisha mwelekeo mwafaka katika hali mpya za utawala wa vijiji na ulimwengu uliotolewa ili kuwezesha mfumo mwafaka ulio na mwelekeo wa nguvu zote (rasilimali, ujuzi, habari, mawazo na kadhalika) kwenye hali yote ya maisha ulimwenguni.

Sisi, Wanainchi wa ardhi, tuna msimamo ya kwamba kubaliano la kiulimwengu la kuchukua sera zilizowekwa katika shawishi hizi lina uwezo wa kusuluhisha janga kwa pamoja na kuunda tamaduni la amani kwa ajili ya vyote vilivyo hai.
Tunaunga mkono uendelezaji wa sera hizi kwenye sharia zilizowekwa pamoja na sera za kimataifa na serikali za mitaa, mashirika na majaribio yaliyoongozwa na wanainchi. Twaheshimu ujuzi wa kitamaduni na kuitaji tamaduni zilete uelewano wa muungano katika utendeaji kwa binadamu na vyote vilivyo hai. Kijipanga karibu na mawanda ya afya ya mtumo kamili inawezesha wanainchi ulimwenguni kujipanga kikamilifu kibinafsi kuelekea kuwezesha maono yaliyokubaliana ya kuinua maisha ya ulimwengu ili:

- Mtandao wa maisha urejeshwe kwenye hali yake ya kawaida iliyo na usawa kukiwa na hewa safi, mchanga ulio na afya, na kufikia maji safi na kukuza ubora wa vyakula vya vyumbe vyote.
- Utandawazi wa jamii unajipanga kulingana na msimo mpya wa kugawana usimamizi ambao waweka afya ya mtumo wote katika kiini chake cha huduma na ada ya mpangilio

- Binadamu hutenda mambo kwa pamoja katika njia ya kuhurumiana na vyumbe ambavyo vinadumisha maisha kwa kusaidia kwenye umoja ambo unabadilika kila mara na kuwezesha mazingara ambayo yaweza kuwezesha kukua na uboreshaji wa maisha kwa vyote.

## PAMOJA TWAINULIWA KIMAISHA

IIDHINISHE MISIMBO

Tafadhali tumia huduma ya kutafsiri kwenye kivinjari chako kutafsiri fomu ya uthibitisho